

Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 03 Issue: 01 | September-2024

EAJK

# Uchanganuzi wa vipashio vya mamlaka katika midahalo ya siasa za uchaguzi wa 2022 nchini Kenya kwenye jukwaa la kidijitali la *youtube*

**Authors**
**Asige Aboge Nelson[(1)]; Miruka Frida[(2)]; Jagero Akinyi Juliet [(3)]**
**Main author email: naasige@gmail.com**

**(1.2) Chuo Kikuu cha MasindeMuliro, Kenya; (3) Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Asige, A. N., Miruka, F., & Jagero, A. J. (2024). Uchanganuzi wa vipashio vya mamlaka katika midahalo ya siasa za uchaguzi wa 2022 nchini kenya kwenye jukwaa la kidijitali la *youtube*. *East Africa journal of Kiswahili*, *3*(1), 33-44. https://doi.org/10.51317/eajk.v3i1.562

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 19.07.2024
Accepted: 02.08.2024
Published: 20.09.2024

Scan this QR to read the paper online

**Copyright**: ©2024 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY) and their terms and conditions.

**Ikisiri**
Makala hii inalenga kutambua mchango wa lugha kama chombo kinachodhihirisha mamlaka katika jamii kwa kuchanganua baadhi ya vipashio vilivyodhihirisha mamlaka katika midahalo ya wakati wa uchaguzi wa 2022 nchini Kenya kama inavyojitokeza katika jukwaa la kidijitali la *Youtube*. Wanasiasa wana hulka ya kutumia lugha yenye kupendeza kwa wananchi nyakati za kampeni kwa njia ya kipekee ili kubadilisha mawazo yao. Katika harakati hizi, wanasiasa huvuta mamlaka upande wao kwa njia isiyo wazi. Hali hii huwafanya wasikilizaji wengi kukosa kuelewa habari iliyotolewa kwa kutoelewa vipashio vilivyotumiwa katika hotuba hizo, hivyo kufanya maamuzi mabaya kisiasa. Utafiti huu ulizingatia muundo wa kiuchanganuzi kwa kutathmini data za kiuthamano zitakazoelezwa kinathari. Eneo la utafiti ni la kitaaluma. Kundi lengwa la utafiti ni midahalo ya wanasiasa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2022 nchini Kenya. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika huku data zikikusanywa kutoka kwenye mtandao wa *youtube* kwa mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo na kuwasilishwa kimaelezo. Makala hii ilibainisha kuwa japo siasa huwasisimua wananchi na midahalo yake kuwavutia kwa wingi, wengi wao hukosa kuelewa kabisa wayasemayo wanasiasa hawa huku wengine wakipata ufasiri potovu. Data zilizokusanywa zitasaidia katika kudhihirisha sababu za wananchi kutoelewa habari fiche ambazo huwasilishwa na wanasiasa katika midahalo yao, ambacho ndicho chanzo cha wananchi kutoelewa habari hizo na hivyo kufanya maamuzi mabaya kwa kuwachagua viongozi wasiofaa.

**Maneno muhimu:** Kampeni, mamlaka, midahalo, vipashio, wanasiasa.

**UTANGULIZI**

Siasa ni ulingo unaohusiana na mizozo. Mizozo hii hujitokeza kwa ujumla bila mpangilio wowote kutokana na matumizi ya lugha. Mizozo hii hulenga kutoa suluhu kwa matarajio ya watu, hasa wananchi, ambao ndio kiini cha kusababisha pingamizi zinazoibuliwa na wanasiasa katika hotuba zao. Ili kusuluhisha mitafaruku, fujo na vurumai, wanasiasa hutumia mamlaka. Fairclough (1989) anahoji kwamba lugha na matumizi yake ni chombo kinachodhihirisha mahusiano ya mamlaka katika jamii. Mamlaka hutokana na ushawishi, matumizi ya ujanja pamoja na mbinu zingine za kubadilisha mawazo ya watu kwa manufaa ya mtu mwingine. Katika mamlaka, mtu au watu fulani humiliki na kuthibiti wengine kitabia au kimawazo. Mthibiti na mthibitiwa hawawezi kuwa na nguvu za namna moja sawia. Kwa hivyo, utousawa katika jamii husababishwa na nguvu hizi. Wakati mwingi, kikundi fulani cha watu wanaowathibiti wengine hufanya na kusema chochote watakacho bila kujali watakachofanya wale wa kikundi kingine.

Mtazamo huu wa Fairclough (keshatajwa) kuhusu mamlaka umechangia makala hii ambayo ilichanganua mamlaka katika midahalo ya siasa za 2022 nchini Kenya kama zinavyojitokeza katika ukumbi wa kidijitali wa *youtube*. Uchaguzi wa 2022 nchini Kenya ulikuwa wa aina yake. Ulihusisha kampeni zilizokuwa na ushindani mkubwa kwa kupiganiwa na wanasiasa wenye ushawishi na uungwaji mkono nchini. Wanasaisa hawa walitumia lugha isiyo wazi na isiyoeleweka kwa urahisi kati ya wananchi. Makala hii imedhihirisha kuwa lugha ya wanasiasa ilivyo wazi kati ya wananchi hudhihirisha mahusiano ya mamlaka ambayo huitaji uchanganuzi wa kindani ili maana iibuliwe.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Swala la mamlaka katika lugha limejitokeza katika muktadha wa lugha ya mahakama. Gibbons (2003) anafafanua kuwa idara ya mahakama ni mojawapo kati ya idara ambazo huweka uzingativu mkubwa katika lugha au misimbo ya lugha inayotumika kortini. Lugha katika muktadha huu hudhirisha mahusiano makubwa ya mamlaka. Katika uhakiki wake alibaini kuwa lugha rasmi ambayo hutumika kortini huhusika na michakato mbalimbali ili kudhirisha itikadi ambayo huzaa mamlaka. Maelezo katika utafiti wake yalidhihirisha kuwa baadhi ya watu kortini huwa na mamlaka kuwapiku wengine na hivyo hutumia lugha kwa namna ya kipekee ili kudhihirisha mamlaka hayo. Gibbons (Kht) aliorodhesha baadhi ya maswali ambayo huulizwa na kujibiwa kortini, na kupitia maswali hayo, hubainika wazi wenye mamlaka pamoja na wale wasio na mamlaka yoyote. Gibbons (Kht) anatupa ilhamu zaidi ya kutaka kuzamia swala hili la mamlaka.

Nafasi ya mwanamke katika jamii ni zao la mahusiano ya mamlaka, Zaja (2008). Mtafiti alijikita katika nyimbo tatu za Taarabu kwa lengo la kubaini namna mambo yanayostahili kuwa siri katika nyimbo hizo hufanywa kuwa wazi kutokana na kuimbwa, kurekodiwa na kusambazwa kwa nyimbo hizo. Zaja (Kht) alihitimisha kwamba uimbaji wa nyimbo za Taarab ni njia ya kudumisha na kuendeleza mapambano ya wanawake dhidi ya mamlaka ya kiume. Mawazo yake yalibainisha suala la uwezo wa kiume wazi. Utafiti wa Zaja (Kht) umetufaa pakubwa kwani mahitimisho yake yamesaidia katika kukuza suala la mamlaka.

Uchanganuzi wa jinsi maana zinavyojenga mahusiano ya mamlaka kati ya wanaume na wanawake ni utafiti uliofanywa na kuhakikiwa naye Matei (2014). Alichunguza mahusiano ya kijinsia katika riwaya ya Unaitwa nani. Katika utafiti wake, Matei (Kht) alibaini kuwa uteuzi wa misamiati na mikakati mingine ya diskosi inayotumika na wasemaji wa kike na wale wa kiume ilidumisha na kukinza mahusiano ya mamlaka. Aliweza kubaini kuwa, mahusiano ya kijinsia yalikuwepo na yalimsawiri mwanamke kama mbebaji wa sifa zinazomwonyesha kama mnyonge, mwovu, mtegemezi miongoni mwa sifa zingine hasi zinazotokana na itikadi ya uwezo wa mwanamme. Mkakati wa uchanganuzi wa kazi yake Matei (Kht) kwa kuzingatia uteuzi wa lugha na misamiati umetufaa sana katika uchanganuzi wetu ambao umezamia vipashio vya lugha ambavyo vimechanganuliwa ili kuibua maana.

Uchanganuzi wa mahusiano ya uwezo yamejitokeza katika utafiti wa Dimbu (2021). Dimbu (Kht) alihakiki uchanganuzi wa diskosi kwa kuzingatia vikatuni vya Shujaaz. Mtafiti alinuia kudhihirisha jinsi mamlaka

ilivyojitokeza kupitia matumizi ya lugha. Ilibainika wazi kwamba mahusiano ya mamlaka yalidhihirika katika vikatuni hivi kutokana na mahusiano katika hadhi mbalimbali za wahusika mashujaa ambao kauli zao zilichukuliwa kwa uzito ikilinganishwa na kauli za wahusika wa kawaida. Wadhamini wa vijana walijitokeza kuwa na uwezo mkubwa kuliko vijana. Watu mashuhuri waliokuwa na ushawishi mkubwa ikilinganishwa na hadhira zao walibainisha uwezo kwa kuzingatia lugha. Katika uhakiki wake, Dimbu (Kht) alibaini kuwa shughuli mbalimbali za kijamii katika mitagusano ya wanajamii huzua mahusiano ya mamlaka hasa kupitia matumizi ya lugha. Alieleza kuwa lugha ndiyo msingi wa ubaguzi katika jamii na huibuka kutokana na mamlaka kati ya wahusika wa kijamii. Makala hii inashabikia maoni ya Dimbu (Kht) kuhusu nafasi ya lugha katika kudhihirisha mahusiano ya mamlaka katika jamii.

## MBINU ZA UTAFITI

Muundo wa Uchunguzi wa Kimaelezo ulitumika katika Uchanganuzi huu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi (U.H.U) Nadharia hii ilibuniwa ili kuratibu majukumu ya lugha katika kutambua uwezo na mamlaka miongoni mwa wanajamii, Malenya na wenzake (2020). Hii ni nadharia inayofungamana na maswala ya kisiasa katika lugha. Katika uchunguzi na uchanganuzi wa matini, nadharia hii hubainisha mamlaka, utabaka na uwezo. Utafiti huu ulizingatia muundo wa kiuchanganuzi kwa kutathmini data za kiuthamano zitakazoelezwa kinathari. Eneo la utafiti lilikuwa la kitaaluma. Kundi lengwa la utafiti ni midahalo ya wanasiasa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2022 nchini Kenya. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika huku data zikikusanywa kutoka kwenye mtandao wa *youtube*. Matokeo nayo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Vipashio vilivyodhihirisha mamlaka katika midahalo ya siasa za 2022

#### Nomino

Maoni mbalimbali yametolewa kuhusu maana ya nomino. Matinde (2012) anaeleza kuwa nomino ni neno ambalo hutaja mtu, kitu, hali, mahali, dhana na tendo. Anadai kuwa nomino ni neno kuu katika kirai nomino ama kiima, huchukua nafasi ya shamirisho au yambwa, ni kijalizo na hutawala utokeaji wa maneno mengine katika sentensi ili sentensi iweze kuwa na muwala wa kisarufi. Matinde anaorodhesha aina mbalimbali za nomino kama: za pekee, za kawaida, dhahania, za makundi, za wingi, kitenzi jina. Katika makala hii, nomino imejitokeza kama kipashio kidhihirishacho mamlaka katika midahalo ya siasa za 2022. Kwa mfano;

**Mfano 1;**

…na nimetumwa na warembo wote wa nchi hii, wamesema
Wale wanatupangia mzee huko kwa hoteli wawache madharau
Bwana, sisi tuko na chuma hapa (akimwashiria Ruto), tunataka
Chuma imesimama sindio? Warembo sindio? Mnataka chuma ya
Kupepetwa ya kulazimishwa kazi? Chuma ni? Chuma ni? Hapo sawa.

Kwa kurejelea diskosi hii ya mwanasiasa Karen Nyamu katika kampeni zilizofanyika Nairobi ili kumpigia debe mgombea urais wa mrengo wa Kenya kwanza, baadhi ya nomino zinajitokeza kuonyesha jinsi alivyovuta mamlaka upande wake na wa mgombea wake. Mwanasiasa huyu anatumia mfano uliofichika na unaweza kuwa mgumu kupata ufasiri kutoka kwa wananchi ambao huenda wasielewe kisemwacho. Nomino ya kawaida mzee imetumika katika diskosi hii kama mtu asiye na uwezo wala ushindani kwani nguvu zimempungua. Hapa, anamrejelea mpinzani kutoka katika mrengo pinzani ambaye, kwa mujibu wa diskosi hii, hastahili kuwa kiongozi wa wananchi kwa kupangiwa urais na 'wale' kwenye mahoteli. Neno wale ni kiwakilishi kinachosimamia wapangaji wa urais katika mahoteli. Kwa kutumia neno lenye kejeli mzee katika hotuba yake, mwanasiasa huyu alinuia kuvuta mamlaka upande wa mgombea kiti wa chama chake. Vilevile, anatumia neno chuma kuleta dhana ya udhabiti wa mgombea wake. Anamwashiria mgombea wake kama chuma ambayo imesimama ili kumaanisha kuwa alikuwa na udhabiti mkubwa ikilinganishwa na mgombea pinzani katika ushindani uliotarajiwa.

Kwa mujibu wa Van Dijk (2000), mamlaka katika jamii na utolewaji wa usemi yana uhusiano. Ni wale wenye mamlaka tu ndio huwa na uwezo wa kutumia semi kwa njia ya kuonyesha udhibiti. Wao hudhibiti miktadha mbalimbali, hadhira zinazowasikiliza, washiriki katika kauli zao na kadhalika. Mfano mwingine wa jinsi nomino imejitokeza kuonyesha udhibiti ni katika hotuba ya Moses Kuria katika kampeni za Kenya Kwanza kule Kiambaa. Tazama mfano ufuatao;

**Mfano 2;**

Na ninataka kuwaambia mbele ya Mungu, if it were not for William Samoei Ruto,
Uhuru Kenyatta would not have been president. That one I can say without the
fear of contradiction. Na ninataka kusema sasa, watu wachague, unataka upande wa
David ama wa Goliath … and I am saying, it is not William Ruto, it is not a movement,
It is a spirit. Ni roho wa Mungu mnapambana naye. And it is not too late mtubu dhambi
na mumuone Bwana. Na mchague vile nimesema, there is no middle ground between
evil and righteousness, between God and Satan, between David and Goliath. Wakati
umefika kuhesabiwa, Mwenyezi Mungu mimi ninataka kuhesabiwa kwa wale
watakatifu wa Hustler nation. Asanteni.

kutokana na diskosi hii, ni wazi kuwa kuna nomino zilizotumiwa ili kuvuta mamlaka upande wa msemaji Moses Kuria. Kwanza, msemaji anatumia nomino ya pekee William Samoei Ruto katika kudhihirisha kuwa isingekuwa yeye, basi Uhuru Kenyatta huenda asingekuwa Rais wa Kenya. Hii ina maana kwamba kati ya Uhuru Kenyatta na William Ruto, ni Ruto aliyekuwa na ushawishi mkubwa zaidi wakati wakishindania mamlaka katika uchaguzi wa 2017 nchini Kenya. Hii inadhihirisha mahusiano ya mamlaka katika upande mmoja kuliko mwingine. Aidha, mzungumzaji anatumia nomino mbili za pekee, David na Goliath. Mazungumzo yake yanahusiana na hadithi ya David katika Bibilia Takatifu, kitabu cha Samueli wa Kwanza, mstari wa 17, ambapo Daudi aliyekuwa mchanga na asiyejulikana kuwa shujaa alimwangamiza shujaa wa Wafilisti, Goliath, katika vita dhidi ya Waisraeli. Kuria anammithilisha William Ruto na Daudi wa Bibilia ambaye tofauti na Mawazo na matarajio ya wengi, alimwangamiza Goliathi, ambaye kwa maongezi yake, ni Raila Odinga, mpinzani wa Ruto. Mfano huu unazidi kushabikiwa na nomino God na nyingine Satan. Kuria anamithilisha William Ruto na Mungu (God) anayejulikana kuwa na mamlaka nyingi kushinda shetani (Satan), ambaye katika diskosi hii, ni mpinzani wa kisiasa wa Ruto, Raila Odinga.

Mifano hii inajitokeza wazi kumletea mamlaka Ruto kwa kudhihaki na kumithilisha mpinzani wake na maovu ya shetani ambaye hapaswi kuchaguliwa. Kumfananisha Ruto moja kwa moja na Roho wa Mungu (Spirit), ni kuonyesha ubabe wake, uwezo na mamlaka yake katika kudhibiti siasa za nchi ya Kenya, na uongozi kwa ujumla.

Kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi, wenye nguvu wanapoongeza na kudhibiti nyenzo na fikra za watawaliwa, hufanya hivyo kwa njia rahisi inayoonekana ya kawaida na isiyo haramu. Ukawaida huu huchangiwa na matumizi ya lugha ambayo husukwa kwa kiwango kikubwa cha ufundi ili kubainisha usawa katika utousawa. Nomino ni mojawapo ya vipashio hivi vya lugha. Kwa mfano, katika kampeni mojawapo za Kenya Kwanza mjini Nakuru, Mgombeaji William Ruto alidokeza;

**Mfano 3;**

"Sisi wote hapa ni mahustler, sisi wote ni waombaji.
Wadosi ndio nyinyi. So, wachana na mheshimiwa sijui nani na nani… because we are building a nation of equals.
Tumekubaliana Nakuru?"

Yale anayoyasema katika usemi huu hayana msingi wa ukweli kwani hakuna jamii ambayo kila mtu ni sawa. Matumizi yake ya Lugha yanajaribu tu kubainisha hali ya usawa katika utousawa. Kuwarejelea wananchi kwa nomino "wadosi" kunadhihirisha wenye mamlaka kuwa wananchi, ilhali inajulikana wazi na wepi ndio wenye mamlaka, ambao ni viongozi. Vilevile, kujirejelea kama "Hustler" kunadhihirisha hali ya usawa kati yake na wananchi, hivyo kudhihirisha maoni ya Van Dijk (2000) kuhusu jinsi usemi wa kisiasa huzua usawa kati ya utousawa. Mzungumzaji anawaonyesha

wananchi wa Nakuru kuwa kila mmoja wao, akiwemo yeye, ni sawa na bali wasiwarejelee viongozi wao kama "mheshimiwa sijui nani na nani."

**Kishazi**

Kwa mujibu wa Fairclough (1993), mchanganuzi wa matini atabaini vipengele vinavyoonyesha mamlaka na Itikadi kwa kuchanganua vigezo vya chini kama misamiati, nomino na vishazi, tena na aendelee hadi vigezo vya juu kama semantiki na pregmatiki. Hivyo basi, vishazi vinajitokeza kuwa kipashio muhimu kilichodhihirika katika midahalo ya wanasiasa katika kampeni za uchaguzi wa 2022. Kibigo (2020) wanaeleza kishazi kama neno au kifungu cha neno chenye kiima na kiarifu au kiarifu pekee ambacho huwa ni sehemu ya sentensi kuu. Maoni ya Matinde (2012) ni kwamba kishazi humilikiwa na kutawaliwa na kifungu kingine cha maneno katika sentensi chenye hadhi kubwa. Anaendeleza kuwa maana ya kishazi hutegemea kifungu kinachokimiliki au kukitawala. Anaorodhesha aina mbili kuu za vishazi: huru na tegemezi.

Katika ushindani kati ya wanasiasa katika kampeni za uchaguzi wa 2022, baadhi ya vishazi vilijitokeza kudhihirisha mahusiano ya mamlaka kati ya wanasiasa, kila mmoja akivuta mamlaka upande wake. Katika kampeni zake Mheshimiwa Raila Odinga, kule Thika, mnamo January 15, 2022, anasema yafuatayo;

**Mfano 1;**

… Kwa upande mwingine, tunaongea ju ya wale watu wetu ambao
hawana chochote, fukara, maskini, hawindi, hohehahe… wanakosa
sabuni, mvua imekosekana mimea imenyauka, njaa imeingia, hakuna
chakula kwa watoto… ata wale walikua wafugaji, na sasa mifugo zinakufa,
ngo'mbe zinakufa, ata mbuzi na kondoo zinakufa. Hakuna chakula
kwa watoto. Wengine wako mjini… Urban poor… amepiga lami,
viatu imetatuka, hana chochote… hatutaki mtoto yetu yoyote alale
na jaa katika taifa letu, ndio sababu tumesema, vile inakua kule Marekani,
kule Ulaya, Kule Brazil, Kule India… tutaleta social protection program,
ili watu wetu ambaye hawana chochote watapata kwa serekali
kila mwezi shilingi elfu sita… Mnaunga mkono? Mnaunga mkono? Eeh?

Kwa kurejelea diskosi hii, kishazi "tutaleta social protection program" kinajitokeza ili kuvuta mamlaka upande wa msemaji. Anajionyesha mbele ya wananchi kuwa suluhu ya matatizo ambayo yanawakumba katika Maisha yao ya kila leo. Anataja baadhi ya matatizo yanayowakumba wananchi katika Maisha yao, wale wa mashambani na mijini, kisha anatoa kauli inayoonyesha kuwa anaelewa matatizo wanayopitia, kwa kusema "hatutaki mtoto yetu yoyote alale na njaa katika taifa letu…". Baadaye anaeleza kuwa ataleta mkakati ambao utasuluhisha tatizo lao. Kishazi hicho ambacho kimemwonyesha yeye kuwa suluhu kimetumika kuvuta mamlaka upande wake ili wananchi wapiga kura wamchague yeye. Vilevile, akizungumza na wananchi wa Nairobi, aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta ambaye aliunga mkono mrengo wa Azimio la umoja alisema yafuatayo;

**Mfano 2;**

… na ndipo mimi nasema, mimi haja yangu… wengine wanawaambia
Uhuru anataka kutawala milele… mimi ninajua mwaka ujao mimi
ninaenda nyumbani, mimi sina shida na hiyo, eeh sina shida,
lakini nia yangu ni kuhakikisha ya kwamba wale ambao wataendelea hawatakuwa watu wa kunyanyasa na kuwaibia wananchi
… watakuwa na hiyo roho ya kuwaunganisha wakenya sio kuwagawanya
wakenya… haja yangu ni wananchi, hao ndio watakuwa mstari wa mbele.

Katika diskosi hii, kuna vishazi vinavyodhihirisha mamlaka upande wa mzungumzaji, huku lawama zikiwaendea wapinzani, na hivyo kuathiri mamlaka yao kwa njia hasi. Msemaji anatumia kishazi "hawatakuwa watu wa kuwanyanyasa na kuwaibia wananchi" kujionyesha kuwa mzuri mbele ya wananchi na

anayejihusisha na wale ambao hawangeweza kuwaibia wananchi wala kuwanyanyasa kwa njia yoyote. Aswani (2013) wanaeleza kuwa msingi wa nadharia ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi ni kuwa lugha yenyewe haina uwezo wala mamlaka, bali hupata uwezo huu kutokana na wanajamii wenye kumiliki uwezo katika jamii husika. Hii ndiyo sababu ya nadharia hii kuchagua mtazamo wa wanaoteswa na kuchanganua kwa kina matumizi ya lugha ya wale wenye uwezo ambao wamewajibika katika kuendeleza hali ya kutokuwa na usawa katika jamii. Hivyo basi, kwa kuwaeleza wananchi kuwa aliwataka wale viongozi wenye roho ya kuwaunganisha wakenya na sio kuwagawanya, alikuwa katika harakati za kuwanyoshea lawama viongozi pinzani akinuia kuwadhibitishia kuwa wanateseka, wamegawanyika, wameibiwa na kunyanyaswa na wanasiasa waliokuwa katika mrengo ule pinzani. Kwa kufanya hivyo, Uhuru alikuwa akivuta mamlaka upande wake huku akiwaonyesha wapinzani kama waovu na wabaya.

Lugha husheheni uwezo. Ni kichocheo cha kudhihirisha na kutathmini mamlaka katika jamii. Vipengele vya lugha hunuia kuendeleza uwezo na mamlaka na hivyo kuongoza mielekeo na matarajio ya wanajamii. Midahalo ya siasa huwa na nafasi kubwa katika uamuzi wanaofanya wananchi wapiga kura. Hii ndiyo sababu wanasiasa huwaongoza na kuwadhibiti wananchi. Akizungumza katika mkutano wa kisiasa mjini Mombasa, Francis Atwoli, aliyeunga mrengo wa Azimio la umoja mkono alitumia lugha ambayo uchanganuzi wake ulidhihirisha mamlaka. Tazama mfano huu;

**Mfano 3;**

…as a responsible trade unionist, I must tell you who is
going to be your president…na siogopi…mimi huyu
mtu anatembeatembea nilimwambia 2014 hautakuwa president…huyu kijana ambaye anadanganya nyinyi alizaliwa
1966 Disemba, mimi 1966 nilikuwa natoka nimemaliza form four,
na wakati huo Watoto wa form four tulikuwa wazee…na baada ya miezi sita nikaandikwa, when he was six months old. If I met the mother I could have been the father! Shenzi!

Katika diskosi hii, kuna baadhi ya vishazi ambavyo uchanganuzi wake unadhihirisha mahusiano ya mamlaka na uwezo wa msemaji na upande wake wa kisiasa. Kwanza, kishazi "I must tell you who is going to be your president" ambacho utafsiri wake ni "Ni lazima niwaeleze ni nani ambaye atakuwa rais wenu" kinavuta mamlaka upande wa msemaji. Hii ni kwa sababu inamdokeza yeye kama mwenye nguvu kiasi cha kujua atakayekuwa rais wa Kenya, hata kabla ya uchaguzi mkuu kufanywa na kura kupigwa. Aidha, Atwoli anamtaja mpinzani mkuu wa mrengo wake kama "kijana ambaye anadanganya nyinyi" kumdhihirisha mpinzani kama mtu mwongo, na asiyefaa kuchaguliwa katika wadhifa wa rais nchini. Vilevile, uchanganuzi wa kishazi "I could have been the father" chenye tafsiri "ningekuwa babake" kinamweka mzungumzaji katika kiwango kikubwa sana cha mamlaka dhidi ya mpinzani anayezungumziwa, ambaye ni William Ruto. Kujimithilisha na babake mpinzani wake kunamtukuza mzungumzaji huku kukinuia kuwafanya wananchi kudhihaki uwezo wa mpinzani wa Azimio kuwa kiongozi wa wananchi. Nadharia ya Uchanganuzi Hakikifu wa Usemi ni utaratibu unaobainisha kategoria za kijamii kwa misingi ya mahusiano yao. Hivi ni kusema kuwa "baba" ataonekana mwenye fahamu zaidi wa anachokisema ikilinganishwa na yule ambaye angekuwa "mwana" iwapo msemaji angekutana na mamake.

**Tamathali za usemi kama vipashio vya mamlaka**

Tamathali za usemi huchukua nafasi kubwa katika uchanganuzi wa lugha. Wamitila (2008) anaeleza kuwa tamathali za usemi ni matumizi mbalimbali ya lugha ambayo hukiuka mtindo uliozoeleka ili kuleta athari au maana fulani. Mitafaruku kati ya wanasiasa yalibainika vilevile kupitia matumizi ya tamathali za usemi. Van Dijk (2000) anadai kuwa wakati wenye uwezo wanapozungumza, wananchi hawana budi ila kuamini na kuchukulia yote asemayo kuwa ya kweli. Wale ambao hawana uwezo, maneno yao hupuuzwa. Hii ndiyo sababu mwanasiasa anapaswa kusuka lugha

ambayo itamwonyesha kuwa mkweli na kuvuta mamlaka upande wake, hivyo kujiweka katika nafasi nzuri ya kupata uungwaji mkono na kuaminika na wananchi wapiga kura.

Katika midahalo ya siasa za 2022 nchini, wanasiasa waliibuka kutumia lugha yenye ustadi na kiwango cha juu usanii. Katika mifano iliyotolewa na wanasiasa, kuliibuka matumizi ya tamathali mbalimbali. Kiini hasa cha matumizi hayo kilikuwa ni kuonyesha ubabe na hivyo kujivutia mamlaka upande wao. Mifano ya tamathali zilizotumiwa ni kama Jazanda, nyimbo, Kejeli, Istiara, Kuchanganya lugha, Makala hii itachanganua baadhi ya tamathali zilizodhihirisha mamlaka katika midahalo tajwa.

**Kejeli**

Kejeli ni mbinu ambayo huchukua nafasi kubwa na kutoa mchango wake si katika mazungumzo tu bali pia katika utoaji wa mawazo yetu ya kila siku, Mrikaria (2010). Katika fasihi, mbinu ya kejeli hutumiwa na waandishi au wasemaji ili kuiwezesha hadhira/wasomaji wafikirie kwa undani suala linaloongelewa ili waweze kupata ujumbe uliokusudiwa kufikishwa kwao. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), kejeli ni mojawapo ya mbinu zinazotawala maongezi yetu hasa kutokana na uwezo wake wa kuficha hisia, maoni na mitazamo yetu sahihi. Aghalabu maneno yanayotumiwa katika kejeli huwa ya kuhusisha hisia, kuchoma, kukata na kutia uchungu. Wanasiasa walitumia kejeli kwa kiwango kikubwa ili kuwafanya wapinzani kuonekana hawana uwezo wa kuongoza na hivyo kuvuta mamlaka upande wao. Kejeli zilizotumiwa ziliwalenga wapinzani moja kwa moja. Tazama mfano ufuatao wa Francis Atwoli akiwa Mombasa huku akimkejeli mpinzani wa mrengo wa Azimio William Ruto;

**Mfano 1;**

…vile nimesema wale wako karibu na William Samoei Ruto,
kule sehemu za Sugoi wakate miti…isiwe karibu ili tarehe
tisa asubuhi siku kura itatangazwa na huyo mtoto atajinyonga…
wakate miti…

kwa mujibu wa Mrikaria (2010), Kejeli hutumia nafasi kubwa katika jamii si katika mazungumzo ya kila siku tu, bali pia namna maoni na mielekeo ya wanajamii mbalimbali inatolewa kimawasiliano. Kwa hivyo, kejeli ni mojawapo ya mbinu zinazotawala mazungumzo ya wanajamii ya kila siku. Kejeli hujengwa katika msingi wa kuwepo na msigano au mgongano wa namna fulani kati ya hali ya maisha na matarajio ya baadae ya wanaohusika. Kwa kujikita katika diskosi hii ya kisiasa, Atwoli anamkejeli William Ruto kwa kutaka wananchi wanaotoka Sugoi, alikotoka mwaniaji huyu wa urais, wakate miti kwa kuwa alikuwa na uhakika wa William Ruto kushindwa katika uchaguzi wa 2022. Kwa kufanya hivi, anadhihirisha mrengo wake kama washindi na hivyo kujiegemeza katika mamlaka kushinda wapinzani wake. Vilevile, Atwoli anamrejelea mwaniaji Ruto kama mtoto ambaye kisiasa hakuwezana na mibabe walioshindana naye. Hii ndiyo sababu ya kusema kuwa "mtoto atajinyonga" katika harakati ya kuwahakikishia wafuasi wa mrengo wake kwamba ushindi ungepatikana upande wao. Kama anavyohoji Mrikaria (keshatajwa), maoni yenye kejeli husalia kuwa vinywani mwa wanajamii kuhusu asasi husika. Hii ndiyo sababu ya msimu "wakate miti" kuzidi kutumika katika kuwakejeli wanamrengo wa Kenya Kwanza, ata kati ya wafuasi wa Azimio la umoja.

Mfano mwingine wa kejeli ulijitokeza katika hotuba ya William Ruto katika harakati ya kujivutia mamlaka wakati wa kampeni za 2022 katika kaunti ya Trans-Nzoia kama ifuatavyo;

**Mfano 2;**

…nilisikia jamaa mwingine, jamaa nilimpatia kazi ya Waziri,
anatoka huku kwenu, ati anasema, ati mimi sijui nilikuwa
nataka kumchapa kofi. Mimi nataka nikawaambie hawa jamaa,
unajua huko kwetu, huko kwetu, hatuchapi kofi wanawake,
sindio? Eeh mmujibu hivyo mumwambie hivyo…

Diskosi hii inadhihirisha kejeli ya kiwango cha juu. William Ruto anatumia jukwaa hili kujionyesha kuwa mwenye nguvu nyingi kwa kudai mbele ya wananchi

kuwa ni yeye aliyempa kazi huyo "jamaa" ambaye kimsingi anayerejelewa ni Eugene Wamalwa aliyekuwa katika mrengo pinzani. Mbali na madai ya kumpa kazi mwanasiasa Eugene Wamalwa, anaendelea kujieleza kwa kumrejelea kama mwanamke. Anaposema kuwa "huko kwetu hatuchapi kofi wanawake" anamrejelea mwanamme ambaye ni mpinzani wake kwa kumdhihaki kuwa yeye si mwanamme. Kwa jinsi hii, mwananchi anapaswa kuwa makini na mwenye ufasiri wa kiwango cha juu ili ajue maana ya usemi na anayerejelewa. Kwa kurejelea suala la utafiti huu, wananchi hukosa kuelewa ama hupata ufasiri potofu kutoka kwa midahalo ya wanasiasa, ambao husuka lugha kwa aina ya kipekee ili kuvuta mamlaka upande wao huku wakiwatwaza wapinzani wao. Wamitila (2008) anaeleza kwamba zipo kejeli ambazo hujengwa kwa matumizi ya maneno tofauti na nyingine ambayo hutegemea mgongano wa hali au jaala.

Istiara

Maana mbalimbali zimetolewa kuhusu istiara na dhima yake katika lugha. Malugu (2021) anahoji kuwa istiara ni mbinu ambayo hujitokeza vitofauti ikilinganishwa na mbinu nyinginezo za lugha mbapo maana hupatikana katika neno. Kwa mujibu wake, istiara hupata maana kutoka kwa kiwango cha miundo au usimulizi. Naye Ogutu (2021) anafafanua istiara kama mbinu ya kulinganisha kitu na kingine, chenye sifa sawa nacho, moja kwa moja bila kutumia vihusishi vilinganishi. Istiara huwa na dhima ya kuibua taswira kuhusu kinachorejelewa. Akimrejelea Wamitila (2003), Ogutu (keshatajwa) anaeleza kuwa maneno kama mithili ya, sawa na na kama hayatumiki katika tamathali hii ya ulinganisho na badala yake, viungo kama "ni" ama "kuwa" hutumika.

Wanasiasa mbalimbali waliibuka katika matumizi ya mbinu ya istiari katika kampeni za uchaguzi wa 2022 kwa lengo la kujilinganisha na ubabe ili kuonekana wababe, na hivyo kuvuta mamlaka upande wao. Alipokuwa Eldoret, Aisha Jumwa huku akimpigia debe mgombea William Ruto, alisema yafuatayo;

**Mfano 1;**

…mimi ndiye shangazi wa taifa, the one and only Mekatilili wa Menza of the 21st century kutoka huko pwani ya Kilifi…

kwa kurejelea diskosi hii, Aisha Jumwa anajilinganisha moja kwa moja na shujaa wa jamii ya Wagiriama, Mekatilili wa Menza, ambaye alipigania uhuru kwa kuongoza jamii yake dhidi ya waingereza ambao walivamia mashamba lao na kuhodhi misingi ya uzalishaji katika jamii hiyo na hivyo kukosa uhuru. Shujaa huyu wa kigiriama aliwakusanya wapiganaji, akawalisha kiapo pamoja na kuwaamuru kupigania uhuru wao. Kwa kujilinganisha na shujaa kama huyu, Aisha Jumwa alinuia kuwaeleza wananchi wa Eldoret kwamba yeye ni shujaa na ikiwa anaweza kuongoza jamii yake kumuunga mkono William Ruto, sembuse wananchi hao wanaotoka katika gatuzi sawa naye Ruto? Matamshi kama haya ni ya kindani na yanahitaji ufasiri kwa undani ili kuibua maana.

Mfano mwingine wa matumizi ya Istiara ulijitokeza katika hotuba ya Raila Odinga kule Mlima Kenya. Tazama mfano huu;

**Mfano 2;**

…wengine walisema ati baba hawezi kupanda mlima, mjue mimi ni tinga, jina yangu nyingine ni tinga, mnajua
tinga? Mnajua tinga? Mlima inaweza kushinda tinga?
Tena mimi sihitaji ruhusa kutoka kwao…mimi sihitaji.
Si nimekuja Mlima kenya?

Katika diskosi hii, mgombea Raila Odinga alikuwa akijilinganisha na Tingatinga kwa kudai kuwa yeye ni mashini ambayo haiwezi kushindwa kupanda mlima. Katika utafiti wake, Ndung'u (2023) anafafanua kuwa nchini Kenya, kulikuwepo maeneo yaliyochukuliwa kuwa yenye ushawishi mkubwa kwa kujiegemeza na mwanasiasa fulani. Anaeleza kuwa eneo la kati liliaminika kumuunga mkono William Ruto kwa wingi na kwamba ilikuwa vigumu sana kwa Raila Odinga kupata uungwaji mkono wa aina yoyote, kwani "hangefaulu kupanda mlima" yenye maana ya kuanguka kura za eneo la kati. Hii ndiyo sababu ya Raila Odinga, katika mfano wetu, kujilinganisha moja kwa moja na tinga ambayo alieleza haiwezi ikalemewa kupanda mlima. Kwa namna hii, Raila alikuwa anavuta mamlaka upande wake kwa kuwaeleza wananchi wapigakura wa eneo la kati kwamba hakuna eneo lolote lililowea kumlemea yeye wala yeyote aliyeweza kumtisha kwa kutaka ruhusa kutoka kwake. Usemi

wake wa kujilinganisha na mashini ni ishara tosha ya mamlaka na uwezo wake kisiasa.

**Jazanda**

Nyongesa (2022) akimrejelea Mbatia (2000) anaeleza Jazanda kama kunga ya utunzi ambapo lugha inatumiwa kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno teule. Kwa njia hii, mtunzi anamwezesha msomaji kuona, kuhisi au kugusa kitu kinachoelezwa. Naye Honora (2010) anahoji kuwa kuna aina tatu kuu za jazanda: za kiubia – zina mbazo zina matumizi duniani kote, za kijamii – zile ambazo zimekubalika kutumika katika jamii fulani pekee na za kibinafsi – zile ambazo kila mtu anapata ufasiri wake binafsi kuihusu. Matumizi ya jazanda yalishamiri katika midahalo ya siasa za 2022 kupitia lugha iliyokuwa fiche na hivyo kuhitaji uchanganuzi wa kina ili kuibua maana. Kwa mfano, mwanasiasa Hassan Omar kutoka Mombasa alisema yafuatayo katika kampeni za William Ruto mjini Eldoret.

**Mfano 1;**

…la mwisho, ya mwisho kabisa, Raila amesema amebakisha
risasi moja, hiyo risasi haikumpata Daniel Moi, risasi hiyohiyo
haikumpata Mzee Kibaki, risasi hiyohiyo haikumpata Uhuru
Kenyatta… nakwambia hiyo risasi yako ni blank na hiyo risasi
haitampata William Ruto… kwa hivyo sisi tunawaomba msimame
pamoja na William Ruto, kama vile sisi tumesimama na Ruto,
tubadilishe Kenya…

Ili kuvuta mamlaka upande wake na ule wa William Ruto, Hassan Omar anatumia jazanda ya risasi moja. Jazanda hii ilipata umaarufu kumrejelea Raila Odinga na uwezo wake wa kuwania uongozi nchini Kenya kwa mara ya mwisho (mara moja). Kwa hivyo, Omar anazungumzia idadi ya chaguzi ambazo Riala alishindwa kumshinda mpinzani wake wa karibu. Anamtaja Daniel Moi ambaye alimshinda Raila katika uchaguzi. Vilevile anawataja Mwai Kibaki na Uhuru Kenyatta ambao walimshinda Raila vilevile, ndiposa akatumia risasi hiyo kama "blank" ambayo tafsiri yake ni "wazi" ambayo kimuktadha ina maana ya isiyoweza kufanya lolote. Kwa jinsi hii, mwananchi wa kawaida anavyoweza kufasiri bila kuzamia kwa undani, maana ya jazanda hii inaweza tu kudhihirika kwa ufasiri wa kina kuhusu maana ya risasi, kwa nini risasi iwe moja, kwa nini itajwe kuwa "blank" na mbona isimlenge Willaim Ruto. Kwa kufanya hivi, Omar alivuta mamlaka upande wa Ruto kwa kuwadhihirishia wananchi wapiga kura kuwa haiwezekani Raila kumshinda Ruto. Aidha, wanasiasa Raila Odinga na Mithika Linturi waliibuka na neno "madoadoa" kutoa maana tofauti katika mikutano tofauti ya kisiasa. Hii inawiana na maoni ya Honora (2010) kuwa kuna baadhi ya jazanda, hasa zile za kibinafsi, ambazo ufasiri wake huwa tofauti kutoka mzungumzaji mmoja hadi mwingine. Katika mkuatno wa kisiasa mjini Wajir, Raila alisema yafuatayo;

**Mfano 2;**

…kuna candidates wengi hapa, wengine wanataka kuwa
magavana, wengine wanataka kuwa senator, tunataka wote hapa Wajir wachaguliwe ndani ya Azimio… hapa Wajir ni Azimio zone, tuko tayari? Tuko tayari?
Hatutaki madoadoa hapa Wajir. Hatutaki madoadoa…

Neno madoadoa katika diskosi hii imetumika kijazanda kutoa maana kwamba watu wa Wajir wasiwachague wanasiasa kutoka katika mirengo mingine. Anadai kuwa watu wa Wajir wawapigie kura wanasiasa wa Azimio na pekee kwa kuwarejelea wanasiasa kutoka mirengo mingine kama madoadoa. Raila hakuwaeleza wananchi moja kwa moja kuwa hakuwataka wanasiasa wa vyama pinzani. Alitumia neno madoadoa. Kwa kufanya hivi, alivuta mamlaka upande wake bila uzingativu wa ikiwa alieleweka au la. Neno madoadoa vilevile lilitumika na mwanasiasa Mithuka Linturi katika kampeni za Kenya Kwanza mjini Eldoret. Tazama mfano ufuatao;

**Mfano 3;**

…Uasin Gishu msicheze na Kenya. Na vile nawaomba, ni kwamba madoadoa yale mliyo nayo hapa, muweze kuyaondoa… hatuwezi kuwa tunasimama na William tukiwa kule Mount Kenya na Meru halafu mko na wengine
hapa hawaskii, hawaungani nayeye…

Katika diskosi hii, mwanasiasa Linturi anatumia jazanda ya Madoadoa kuleta dhana ya wapinzani wa William Ruto katika eneo la Uasin Gishu. Anasema kuwa watu wa Uasin Gishu wawaangushe wanasiasa wengine wote ambao hawaungi azma ya William Ruto mkono. Kwa kufanya hivi, anavuta mamlaka upande wa William Ruto kwa kumwonyesha kuwa mkuu na mtawala zaidi ya viongozi wengine wote. Anamithilisha kuwaunga mkono "madoadoa" kama "kucheza na Kenya" na hivyo kumweka kingozi Ruto katika ulingo wa juu zaidi kimamlaka.

**Takriri**

Kwa mujibu wa Kamusi teule ya Kiswahili (2019), takriri ni mbinu ni tamathali yenye usemi wenye urudiaji wa jambo moja kwa njia tofauti. Uhusu urudiaji wa maneno, irabu, silabi au fungu la maneno katika sentensi. Maelezo haya yanawiana na maoni ya Wamitila (2008) anayeeleza takriri kama urudiaji wa sauti, neno au sentensi fulani, pia hujulikana kama uradidi. Nia ya mtumiaji au mtunzi wa mbinu hii huwa ni kuleta msisitizo. Wanasiasa katika midahalo yao wakati wa kampeni walitumia mbinu hii hasa ili kusisitiza kwa wananchi maneno yatayokolea akilini mwao ili kupata uungwaji mkono. Nia kuu ya wanasiasa kutumia mbinu hii ni ili kuvuta mamlaka upande wao kwa kukoleza maneno akilini mwa wananchi kwa msisitizo. Fairclough (1989) anaeleza kuwa udhibiti wa fikra za umma ni sifa moja ya wanasiasa kujivutia mamlaka. Katika mkutano wake kujiimarisha kule Butsotso, kaunti ya Kakamega, William Ruto alisema yafuatayo;

**Mfano 1;**

…ati wako na deepstate na system, wataninyanganya kura.
Mimi nataka muniangalie, nyinyi watu wa Butsotso, nyinyi
mkiona, mimi ni mtu ya kunyanganywa kura kweli? Yaani
mkiniona hivi, mimi ni mtu ya kunyanganywa kura? Sisi tulishindana nao kule Msambweni, si tuliwashinda? Si tulishindana nao Juja, si tuliwashinda? Si tulishindana nao
kule Kiambaa, si tuliwashinda? Hii tarehe tisa mwezi wa
nane tutawashinda asubuhi na mapema…

Mwanasiasa William Ruto anawazungumzia wananchi wa Butsotso kwa msisitizo kwa kutumia mtindo wa takriri kuvuta mamlaka upande wake kwa kuwasisitizia kuwa yeye si mtu wa kunyanganywa kura. Maoni yake yanaegemea maoni ya wanasiasa wa awali kuhusu tetesi za wizi wa kura ili kumpendelea mpinzani wa kisiasa wa Ruto, Raila Odinga. Mzungumzaji anajiinua juu ya wapinzani kwa ubabe kwa kuwauliza wananchi wa Butsotso mara kadhaa kuhusu ikiwa wanadhani yeye ni mtu anaweza kuibiwa kura. Maelezo yake yanawafanya wananchi kumjua kama mtu ambaye anayafahamu mengi ya kisiasa na kwamba hakuna uwezekano wa aina yoyote kwa mtu mwingine kumnyanganya mamlaka kupitia wizi wa kura. Anaendeleza hotuba yake kwa kurudiarudia chaguzi mbalimbali ambazo chama chake kilishinda dhidi ya chama cha mpinzani wake wa urais katika uchaguzi na kutoa madai kuwa alishinda chaguzi zote zile. Kwa kufanya hivi kwa msisitizo, mzungumzaji alikuwa akidhibiti fikra na maoni ya wananchi ili kujiweka katika kilingo cha juu kabisa cha mamlaka.

Udhihirikaji wa mbinu ya takriri unabainika vilevile katika usemi wa Babu Owino katika kampeni za Azimio la Umoja mjini Kisumu. Tazama mfano ufuatao;

**Mfano 2;**

**Kiingereza**

…For something good to happen, another thing must break. For a seed to germinate, the ground must break. For a woman to give birth, water must break. For a woman to enjoy full potential of her anatomy, her virginity must break. For it to rain, the clouds must break…therefore, for the price of unga to reduce, the dictatorial government, the autocratic government, the rutocratic government must break. For the price of fuel to reduce, the rutocratic government must break…

**Tafsiri**

…Ili jambo zuri litokee, jambo lingine lazima livunjike. Ili mbegu iote, ardhi ni lazima ivunjike. Ili mwanamke azae, maji lazima yapasuke. Ili mwanamke afurahie uwezo kamili wa umbile lake, ubikira wake lazima uvunjike. Ili mvua kunyesha, mawingu lazima yapasuke…kwa hiyo, ili bei ya unga ipungue, serikali ya kidikteta, serikali ya kiimla, serikali ya kiruto lazima

ivunjike. Ili bei ya mafuta ipungue, serikali ya kiruto lazima ivunjike…

Mfano huu wa matumizi ya takriri unadhihirisha msisitizo wa Babu Owino kuwa ili nchi ya Kenya isuluhishe matatizo yake, basi wakenya hawana budi ila kujizuia kumpigia kura kiongozi mpinzani William Ruto. Anasisitiza kwa mifano anuwai kuwa ili vitu vizuri kama mbegu, uzazi, mvua na kadhalika kupatikana, basi lazima kingine kivunjwe. Kwa kutumia mfano huu, mwanasiasa huyu anaeleza wananchi kuwa kumwangusha William Ruto ndiko suluhisho kwa matatizo yanayowakumba. Anamdunisha mpinzani wake zaidi kwa kutumia neno "rutocratic" pamoja na "udikteta" na "uimla" ili kumpaka rangi ya uovu na ukatili ili wananchi wasimpigie kura. Kwa kufanya hivi, ingawa baadhi tu ya wasikilizaji ndio walielewa alichokisema kwa jinsi alivyokisema, kusudio lake lilikuwa ni kuvuta uwezo na mamlaka upande wa mwaniaji wake wa urais, Raila Odinga.

**HITIMISHO:** Makala hii imebainisha kuwa japo siasa huwasisimua wananchi na midahalo yake kuwavutia kwa wingi, wengi wao hukosa kuelewa kabisa wayasemayo wanasiasa hawa huku wengine wakipata ufasiri potovu. Katika midahalo ya wanasiasa ambayo tumechanganua, imejitokeza kuwa wanasiasa hawa wanapozungumza husuka lugha kwa njia ya aina yake huku wakivuta mamlaka upande wao kwa njia isiyo wazi. Katika harakati hizi, hupata uungwaji mkono kwa wingi huku wapinzani wakishushwa mamlaka. Kwa kutofahamu, wananchi hufanya maamuzi yasiyofaa kwa kuwachagua viongozi hawa kwa kufuata walichokisema ambacho hakikueleweka vyema. Lugha imetumika kama chombo cha kudhihirisha mamlaka, huku vipashio vyake kama nomino, vishazi na tamathali mbalimbali zikidhihirisha mahusiano ya kiuwezo. Hali hii inadhihirisha lugha kama chambo cha kukuza na kuendeleza matakwa ya wenye uwezo ikilinganishwana wale wasio na uwezo. Uchanganuzi umegundua kuwa lengo kuu la mwanasiasa ni kusaka mamlaka kwa njia yoyote, kwa kutumia ukweli ama uongo, na kusuka lugha kwa njia spesheli ili kufaa azma yake. Anahakikisha kwamba mahusiano ya kiitikadi kati yake na mwananchi mpiga kura yanahifadhiwa katika kiwango cha mwananchi kukosa mamlaka na hivyo kudhihitiwa na matakwa ya mwanasiasa.

**MAREJELEO**


Aswani, B. (2013). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Serengeti Educational Publishers.

Dimbu, S. L. (2021). Mdhihirisho wa Mahusiano ya Uwezo katika Vikatuni vya Shujaaz: Uchanganuzi Makinifu wa Kidiskosi. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, *5*(2), 40-57.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. Longman.

Fairclough, N. (1993). Critical Discourse Analysis and the Marketization of Public Discourse: *The Universities. Discourse and Society*, *4*, 133-168.

Gibbons, J. (2003). *Questioning in Common Law Criminal Courts*. University of Western Sydney.

Honora, F., & Susan, S. (2012). *The reporter Who died Probing*. Amazon

Kibigo, M. L. (2020). *Ubabedume katika majigambo ya miviga ya Shilembe na mchezasili wamayo miongoni mwa waisukha nchini Kenya kwa mtazamo wa kisemantiki*. Masinde Muliro University.

Malenya, M. M., Wandera-Simwa, S. P., & Ogola, J. O. (2020). Itikadi na uwezo wa kijinsia katika nyimbo za Taarab. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, *2*(1), 48-60.

Malugu, A. (2021). Istiara katika Riwaya ya'Kusadikika'ya Shaaban Robert. *Mwanga wa Lugha*, *6*(1), 55-66.

Matinde, R. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia*: *Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mbatiah, M. (2000). *Kamusi ya Fasihi*. Standard Text Books Graphics & Publishing

Mrikaria, S. E. (2010). *Kejeli na fasihi ya Kiswahili-Tanzania*.University of Leipzig

Mulila-Matei, A. K. (2014). *Discourse, gender identity and gender Power relations in Fiction: A Critical discourse Analysis and Systemic Functional grammar reading of Wamitila's Unaitwa Nani?* Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ndung'u, R. (2023). Ethnicised politics in Kenya.Journal of Central and Eastern European African Studies, *3*(1), 121-129.

Nyongesa, N. (2022). Matumizi ya jazanda katika uwasilishaji wa mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Kithaka wa Mberia. *Research Journal in African Languages*, *3*(3).

Ogutu, H. O. (2021). Uchunguzi wa fani za lugha zilivyotumika kuibua changamoto za vijana katika riwaya teule za Kiswahili. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, *3*(1), 199-210.

Van Dijk, T. A. (2000). *Critical Discourse Analysis. Discourses in Society website*. https://www.discourses.org/OldArticles/Critical%20discourse%20analysis.pdf on 3/8/2018.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers.

Zaja, J. O. (2008). *Publicizing the Private: Feminist Locution in Taarab Songs and performance.* University of Nairobi.